## UTOAJI WA HUDUMA ZA KANSA/SARATANI

| DARAJA YA HUDUMA | MAWANDA YA HUDUMA ZINAZOTOLEWA |
|---|---|
| Daraja 1 (Jamii) | Kuhamasisha kuhusu afya bora |
| Daraja 2 (Zahanati) | Kuimarisha Afya; Kupima; Kugundua kansa mapema |
| Daraja 3 ( Vituo vya Afya) | Kuimarisha Afya ; Kupima ; Kugundua kansa mapema |
| Daraja 4 (Vituo vya Msingi vya Rufaa) | Kuimarisha Afya; Kupima; Kugundua kansa mapema; Kutibu (Upasuaji,Kemotherapia, Msaada); Msaada, Kupunguza maumivu |
| Daraja 5 (Vituo vya Upili vya Rufaa) | Kuimaridha Afya; Kupima; Kugundua kansa mapema; Kutibu (Upasuaji, Kemotherapia, Radiotherapia; Msaada; Kupunguza maumivu. |
| Daraja 6 (Vituo vya Juu vya Rufaa) | Matibabu maalum (Upasuaji, Kemotherapia, Radiotherapia, Imiuonotherapia, urekebishaji) Utafiti, Mafunzo |

### Huduma za punguzaji wa Maumivu

Hizi ni huduma zinazolenga kuimarisha ubora wa maisha ya wagonjwa na familia zao. Huduma hizi ni pamoja na : Ushauri nasaha, Kudhibiti huzuni baada ya kufiwa na wapendwa, Kuimarisha Lishe, Udhibiti wa pesa, Udhibiti wa athari hasi za matibabu, Mitazamo mbalimbali ya kifamilia, Msaada kutoka kwa watu wengine. Huduma hizi hutolewa tangu mwanzo wa kuanza kuugua kansa na katika safari nzima ya kukabiliana na ugonjwa huo.
Kwa taarifa zaidi, wasiliana na afisa wa afya

### Wanaounusurika

Wanaonusurika kutokana na kansa, wahudumu wao n wanapaswa kuyaona maisha katika ukamilifu wake na wala si kujikita katika kansa na athari zake pekee. Ili kufanikiwa kufikia lengo hilo, wanaweza kuangazia vipengee vingine (Mazoezi, Masuala ya Kijamii, Fedha, Saikolojia, Imani, Elimu).

## HOSPITALI ZINAZOTOA HUDUMA ZA KANSA NCHINI KENYA

| Eneo | Hospitali | Umiliki | Kiwango cha matibabu |
|---|---|---|---|
| Nairobi | Hospiali ya Kitaifa ya Kenyatta | Serikali | Kituo cha Matibabu Kamilifu ya Kansa |
| Mkoa wa Kati | Hospitali ya Mafunzo ya Rufaa ya Chuo Kikuu cha Kenyatta | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| | Hospitali ya Kijabe | Kanisa/Dini | Kituo cha Matibabu ya Kimsingi ya Kansa |
| | Hospitali ya Kaunti ya Nyeri | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| | Hospitali ya Misheni ya Mathari Consolata | Serikali | Essential Cancer Centre |
| | Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Meru | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| | Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Embu | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| Magharibi na Nyanzai | Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Kakamega | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| | Hospitali ya Mafunzo ya Rufaa ya Jaramogi Oginga Odinga | Serikali | Kituo cha Matibabu ya Kimsingi ya Kansa |
| Pwani | Hospitali ya Coast General | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| | Hospitali ya Rufaa ya Moi Voi | Serikali | Kituo cha Matibabu Kamilifu ya Kansa |
| Bonde la Ufa | Hospitali ya Rufaa ya Longisa | Serikali | Kituo cha Matibabu Kamilifu ya Kansa |
| | Hospitali ya Misheni ya Tenwek | Serikali | Kituo cha Matibabu ya Kimsingi ya Kansa |
| | | Kanisa/Dini | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| | Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Nakuru | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| Kaskazini Mashariki | Hospitali ya Rufaa ya Garissa | Serikali | Kituo cha Matibabu Kamilifu ya Kansa |
| Nyanda za Chini Mashariki | Hospitali ya Rufaa ya Makueni | Serikali | Kituo cha Matibabu Kamilifu ya Kansa |
| | Hospitali ya Rufaa ya Machakos | Serikali | Kituo cha Kati cha Matibabu ya Kansa |
| Nyanda za Juu Mashariki | | Serikali | Kituo cha Matibabu ya Kimsingi ya Kansa |

National Cancer Institute of Kenya
NCI - KENYA

## TAASISI YA KITAIFA KUHUSU KANSA - KENYA (NCI_K)

Hii ni taasisi iliyobuniwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kudhibiti Kansa ya Mwaka 2012, kushirikisha na kuratibu ukingaji, matibabu na udhibiti wa kansa nchini Kenya.

### MAONO

Kuwa kwenye msitari wa mbele duniani katika, kukikinga na kudhibiti kansa

### DHAMIRA

Kusimamia utoaji wa viwango vya juu , kutegemea ushahidi katika kinga dhidi ya kansa, udhibiti wake kwa kushirikiana na asasi nyingine, kutafiti, kubuni sera, kuratibu na uhamasishaji.

*Kuwa Msitari Wa Mbele Kukabiliana Na Kansa*

Kwa taarifa zaidi, wasiliana nasi kupitia:


Kituo: National Cancer Institute of Kenya
Landmark Plaza 6th Floor
P.O.Box 30016 00100 Nairobi. Kenya
Barua pepe: ncikenya@gmail.com
Simu: (+254) 795 012 568, 717 389 120
Wavuti: www.ncikenya.or.ke
Twita: @NCIKenya


Au
tembelea ofisi zetu katika jumba la
Landmark Plaza , 6th floor, Argwings Kodhek Road

JAMUHURI YA KENYA

National Cancer Institute of Kenya
NCI - KENYA

# UNAYOPASWA KUJUA KUHUSU KANSA/SARATANI

*Tuzungumze Kuhusu Kansa*

## Kansa/Saratani ni Ugonjwa gani?

Kansa, saratani au uvimbe ni ugonjwa ambapo seli au chembechembe za mwili hukua kwa kasi na kwa njia isiyo ya kawaida na kusambaa hadi viungo vya mwili na kuathiri utendakazi wao. Kuna aina mbalimbali za kansa.

*"Kansa si uchawi, laana au dhambi"*

## Kansa husababishwa na nini?

Chanzo cha ugonjwa wa kansa hakijulikani hasa. Hata hivyo, kuna hali na mitindo ya maisha ambayo inaweza kuchangia uwezekano wa mtu kuugua kansa. Hali hizi ni pamoja na :

- Mtindo wa maisha kama vile matumizi ya tumbako, pombe, lishe isiyo bora na kutofanya mazoezi ya mwili na kadhalika.
- Aina fulani za maambukizo.
- Mfumojeni wa mtu na historia ya familia kuhusiana na ugojwa wa kansa.
- Hali ya mazingira,hasa mtu anapotangamana na miale na kemikali hatari au zenye sumu kwa mfano asibestosi.

Utumizi wa tumbako



Utumizi wa pombe



Lishe isiyo bora



Kutofanya mazoezi




## Unawezaje kujikinga dhidi ya kansa?

Kwa kuwa chanzo cha kansa hakijulikani hasa, hakuna njia mahususi za kujikinga dhidi ya ugonjwa huu. Hata hivyo, njia zifuatazo zinaweza kufuatwa ili kupunguza uwezekano wa kuugua kansa:

- Jiepushe na miale hatari, sumu zitokanazo na shughuli za viwandani na mazingira mengine.
- Jikinge kutokana na miale ya jua au tumia vifaa vya kujikinga dhidi ya miale hiyo.
- Pata chanjo dhidi ya Virusi vya Papiloma ya Binadamu na (HPV) na Hepatitisi B (Hep B).
- Jiepushe na ngono kiholela au ngono bila kinga.
- Fanyiwa na matibabu mara kwa mara.
- Fanya mazoezi ya mwili mara kwa mara
- Jiepushe na matumizi ya tumbako
- Jiepushe kunywa pombe

## Ishara Za Wazi Za Kansa Ni Zipi?




## Aina za kansa zinazo fahamika na watu wengi kenya ni zipi?

Aina za kansa zinazofahamika na wengi nchini kenya kwa mujibu wa data ya Globocan 2020 ni pamoja na:

1. Kansa ya matiti
2. Kansa ya mlango wa kizazi (seviksi)
3. Kansa ya tezi (prosteti)
4. Kansa ya Koo/umio
5. Kansa ya utumbo/rektamu

### Ishara za jumla za ugonjwa wa kansa

Ishara na dalili za mapema za kansa zinazofahamika sana ni pamoja na:

- Kubadilika kwa mazoea ya kukojoa na kunya
- Kidonda kisichopona
- Uvujaji damu au kutokwa na uchafu usio wa kawaida.
- Uvimbe au bonge kwenye matiti au au sehemu nyingine mwilini.
- Matatizo katika kwenda choo au kuvimbiwa.
- Mabadiliko ya wazi ya ngozi yasiyokuwa ya kawaida
- Kikohozi kiachosumbua

### Aina za Kansa zinayoathiri Watoto

- Leukemia (Kansa ya damu)Cancer of the blood)
- Limfoma kwa mfano Limfoma ya Burkitts
- Uvimbe au Tyuma katika mfumo wa neva za uti wa mgongo

### Ishara wazi za kansa miongoni mwa watoto

Ishara na dalili za mapema za kansa miongoni mwa watoto ni pamoja na:

- Kupungua kwa uzito kwa njia isiyoeleweka
- Kuumwa na kichwa na kutapika asubuki.
- Kuvimba na maumivu makali kwenye mifupa, vifundo, mgongo au miguu.
- Uvimbe au bonge, hasa katika tumbo, shingo, Kifua, nyonga au kwapani.
- Upele kwenye ngozi unaovuja damu.
- Maambukizo ya mara mara
- Rangi nyeupe nyuma ya mboni ya jicho.
- Kuongezeka kwa kichefuchefu au kutapika bila kuhisi kichefuchefu.
- Uchovu wa mara kwa mara aukufifia kwa ya rangi ya ngozi
- Kushindwa kuona vizuri kunakotokea ghafla na kukithiri.
- Homa inayokithiri ambayo chanzo chake hakijulikani.

**Endapo utakumbwa au kushuhudia ishara hizi, chukua hatua za dharura. Tembelea Kituo cha afya kilicho karibu nawe kupata taarifa zaidi pamoja na kufanyiwa uchunguzi.**

## Kwa nini unapaswa kufanyiwa uchunguzi wa dalili za kansa?

Uchunguzi wa kansa ni ukaguzi unaofanywa kubainisha kuwepo au kutokuwepo kwa kansa.

- Wasiopatikana na ugonjwa huu wanapaswa kuendelea kujiwekea tahadhari ili kupunguza uwezekano wa kuugua kansa. Hata hivyo, mtu anapaswa kuendela kufanyiwa ukaguzi wa mara kwa mara.
- Wanaopatikana na ugongwa huu, ugunduzi wa mapema ni muhimu ili kuwezesha ugonjwa huu kudhibitiwa.

## Ni aina gani za kansa zinazopaswa kufanyiwa Uchunguzi?

Aina zifuatazo za kansa zinaweza kufanyiwa uchunguzi:

- Kansa ya matiti
- Kansa ya Mlango wa kizazi
- Kansa ya tezo (Prosteri)
- Kansa ya ngozi
- Kansa ya utumbo na rektamu
- Kansa ya Kinywa
- Kansa ya koo/umio
- Kansa ya Mapafu
- Kansa za watoto kwa mfano kansa ya macho na uvimbe

## Hatua gani ichukuliwe baada ya kupatikana na kansa?

- Muulize mhudumu wa afya kuhusu aina ya kansa unayougua na kiwango cha maenezi yake.
- Pewa taarifa kuhusu matibabu ya aina kansa unayougua
- Fahamu mahali ambapo unaweza kupata huduma za matibabu
- Fahamu mpango , muda na malengo ya huduma za matibabu.
- Fahamu athari hasi zinazosababishwa na matibabu
- Wafahamishe jamaa na marafiki kwa minajili ya msaada
- Tafuta taarifa kuhusu jinsi kuugua kansa kutakavyoathiri shughuli zako za kila siku.
- Hakikisha kwamba ada yako ya Hazina ya Bima ya Afya (NHIF)imelipwa ipasavyo.
- Tafuta mtu atayekuwa anaandamana nawe kwenda hospitalini kwa minajili ya huduma za matibabu.
- Jiunge na kikundi cha waathiriwa wengine wa kansa ( watu wenye hali sawa na yako)
- Muulize muhudumu wa afya maswali maswali yoyote unayoweza kuwa nayo.



**WITO WA HATUA**

**Kupimwa kansa huokoa MAISHA**

(Nenda upimwe kansa Leo)

## Kansa inadhibitiwa vipi?

Kutegemea hali, viwango na sifa za kansa, aina zifuatazo za matibabu hutolewa na wahudumu wa afya.

1. Upasuaji: Kuondoa tishu zenye kansa kwenye viungo vya mwili.
2. Radiotherapi: Tiba ya kansa kutumia miale ionisha au eksi-rei. Miale hii huua seli za kansa na kudidimisha uvimbe.
3. Kemotherapi/Tibakemikali: Tiba kwa kutumia dawa au kemikali ambazo zinadhuru vimelea vinavyosababisha kansa.
4. Therapi ya homoni: Kutibu kansa kwa kutumia dawa zinazositisha kukua kwa seli za kansa.
5. Imiunotherapi: Kutibu kansa kwa kutumia dawa zinazochochea kuimarika au kudidimiza kinga ya mwili ili kuusaidia kukabiliana na ugonjwa huo.